# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## Tuzifahamu Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki,

### Utangulizi

Tanzania imetangaza kupiga marufuku kutengeneza, kusambaza, kutumia au kutunza mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 1 Juni mwaka 2019. Katazo hili linafuatia tangazo lililotolewa na Waziri Mkuu na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Katazo la mifuko ya plastiki ni utekelezaji wa kifungu cha 230 (2)(f) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Tangazo la katazo la mifuko ya plastiki limeanza utekelezaji kwa kutungwa kwa Kanuni husika za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za mwaka 2019. Kanuni hizi zilitangazwa na Waziri wa Ofisi ya Makamu ya Rais Mambo ya Muungano na Mazingira, Mh. Januari Makamba ambazo zimeanza kutumika terehe 1 Juni 2019.

### Madhumuni ya Kanuni

Kanuni husika za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za mwaka 2019 kwa kifupi zina madhumuni yafuatayo:

a) Kupiga marufuku uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki bila kujali unene wa mifuko hiyo;
b) Kulinda afya ya binadamu na wanyama pamoja na mazingira dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya mifuko ya plastiki;
c) Kutoa motisha kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji na uingizaji wa mifuko mbadala.

### Je, Ni mifuko ya Aina Gani ya Plastiki inayopigwa Marufuku?

Kanuni zinapiga marufuku vitu vifuatavyo:

i. Mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali;
ii. Vifungashio vya plasiki vinavyotumika kuuza vinywaji au bidhaa nyingine, isipokuwa tu kama aina ya bidhaa hizo inalazimu kutumia vifungashio vya plastiki;
iii. Kusajili au kutoa leseni au kibali kwa mtu yeyote kwa ajili ya kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha au kuuza mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku kwa mujibu wa Kanuni hizi;


**Board of Directors:**
**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**

**Je mifuko ya plastiki na vifungashio vya plastiki ni nini?**

i. Mfuko ya plastiki ni mfuko uliotengenezwa kwa malighafi ya plastiki wenye vishikio au bila vishikio ambao una unene wa aina yoyote kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali.

ii. Vifungashio vya plastiki ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki kwa ajili ya kuhifadhia ubora au kuzuia uharibifu wa bidhaa ambavyo vitakuwa na lakiri au alama inayotambulisha bidhaa iliyofungashwa kabla ya kuuzwa, kusambazwa au kuingizwa sokoni.

**Je, Ni Matumizi Gani Yanaruhusiwa?**

Kanuni hizi hazijapiga marufuku bidhaa zote za mifuko ya plastiki, bali imeainisha baadhi ya bidhaa ambazo hazijapigwa marufuku. Bidhaa hizi ni vifungashio vya plastiki kwa ajili ya huduma za afya au bidhaa za viwandani au sekta za ujenzi, kilimo au vyakula au usafi na udhibiti wa taka. Kanuni zinataka matumizi ya vifungashio hivi kuhakikisha kuwa takataka zitokanazo na matumizi ya vifungashio hivi zinasimamiwa au kutupwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

**Makosa na Adhabu za Ukiukwaji wa Kanuni**

Ni makosa kwa mtu yeyote kuingiza nchini au kusafirisha nje ya nchi au kuzalisha au kuuza au kusambaza au kumiliki au kutunza mifuko ya plastiki na vifungashio vya plastiki ambayo imepigwa marufuku kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Kanuni zimeweka adhabu mbalimbali za ukiukwaji wa kanuni hizi za marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kuzalisha au kuingiza nchini mifuko ya plastiki, na adhabu yake ni faini ya kati ya shilingi milioni 20 mpaka bilioni moja au kifungo cha miaka miwili au zaidi jela.
2. Ni kosa kusafirisha nje ya nchi mifuko ya plastiki, na adhabu yake ni faini kati ya chilingi milioni tano hadi milioni ishirini; au kifungo kisichozidi miaka miwili; au vyote kwa pamoja.
3. Ni kosa kuhifadhi au kusambaza mifuko ya plastiki, na adhabu yake ni faini ya kati ya shilingi milioni tano mpaka milioni 50; au kifungo kisichozidi miaka miwili, au vyote kwa pamoja.
4. Ni kosa kuuza mifuko ya plastiki, na adhabu yake ni faini ya kati ya shilingi laki moja mpaka laki 5; au kifungo kisichozidi miezi mitatu; au vyote kwa pamoja.
5. Ni kosa kumiliki au kutumia mifuko ya plastiki na adhabu yake ni kati ya shilingi elfu 30 hadi laki mbili; au kifungo kisichozidi siku saba; au vyote kwa pamoja.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member,
Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member,
Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

**Ni Taasisi Gani Zinahusika katika Utekelezaji wa Matakwa ya Kanuni**

Taasisi zifuatazo zimepewa jukumu la utekelezaji wa Kanuni hizi:

a) Waziri husika wa mambo ya mazingira Tanzania Bara ambaye ana jukumu la kutoa miongozo na maelekezo juu ya utekelezaji wa Kanuni hizi;
b) Baraza la Taifa la Usimamizi wa mazingira ndilo baraza la kwanza la rufaa;
c) Taasisi nyingine yoyote ya serikali kama Wizara, Idara na Wakala wa Serikali;
d) Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na mamlaka yake ya uteuzi;
e) Maafisa wa Mazingira walio chini ya Baraza la Taifa la usimamizi wa Mazingira (NEMC).

**Je, Masharti ya Jumla ya Kanuni ni Yapi?**

Kanuni zimeweka masharti ya jumla kama ifuatavyo:

i. Kurudisha mifuko ya plastiki kwenye nchi ilikotoka kwa gharama za mwagizaji, pale itakapopatikana katika kituo chochote mpakani.
ii. Utaifishwaji, kutupa na kuteketezwa au kurejelezwa kwa mifuko ya plastiki kwa kutumia njia zilizo rafiki kwa mazingira kwa gharama za mtenda kosa.
iii. Mzalishaji au msambazaji wa bidhaa zilizofungashwa katika chupa za plastiki ataweka utaratibu wa mfumo wa ukusanyaji wa taka za chupa hizo kwa ajili ya kurejeleza na haruhusiwi kuongeza bei kwa mlaji ili kufidia gharama hizo.
iv. Mtu akionyesha nia ya kulipa kiasi cha pesa kama faini ya ukiukaji wa Kanuni basi kosa lake hilo linaweza kufifilishwa.

**Je ni amri gani nyingine zinaweza kutolewa na mahakama kwa ukiukwaji wa Kanuni?**

i. Amri ya kutaifisha mifuko ya plastiki;
ii. Amri ya kufunga kiwanda kinachozalisha mifuko ya plastiki;
iii. Amri ya kufuta leseni; au
iv. Kuamrishwa kushiriki katika kutoa huduma za kijamii.

**Endapo mtu hajaridhishwa na maamuzi anaweza kukata wapi rufaa?**

i. Mtu yeyote ambaye hakuridhishwa na uamuzi uliotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi, isipokuwa Mahakama, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini kutoka siku ya maamuzi.
ii. Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na uamuzi uliotolewa na Waziri anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa la Mazingira ndani ya siku thelathini kwa namna ambavyo itawekwa na Baraza.

**Board of Directors:**
**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**